Wizara ya Kazi ya Marekani

Matokeo ya Mwaka 2019 juu ya Aina Mbaya Sana za Ajira kwa Mtoto

Tanzania

Mnamo mwaka 2019, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya maendeleo kidogo katika juhudi za kutokomeza aina mbaya sana za ajira kwa mtoto. Maafisa wa polisi wa sheria ya makosa ya jinai walishtaki, walifanikisha hukumu, na kutolewa adhabu ya vifungo kwa kesi mbili zilizohusiana na aina mbaya sana za ajira kwa mtoto. Hata hivyo, licha ya juhudi mpya kushughulikia ajira kwa mtoto, Tanzania inapokea tathmini ya maendeleo duni kwa sababu iliendelea kutekeleza zoezi ambalo lilichelewesha maendeleo katika kutokomeza aina mbaya sana za ajira kwa mtoto. Serikali ya Bara inaunga mkono waziwazi kufukuzwa kwa kawaida kwa wanafunzi wajawazito kutoka katika shule za umma, huku ikiwafanya kuwa katika mazingira hatarishi ya aina mbaya sana za ajira kwa mtoto. Watoto nchini Tanzania hushiriki katika aina mbaya sana za ajira kwa mtoto, ikiwa ni pamoja na uchimbaji madini, upasuaji wa mawe na kazi za majumbani, kila mojawapo mara nyingine inapelekea biashara ya usafirishaji haramu wa binadamu. Watoto pia hufanya kazi za hatari sana katika kilimo. Mapungufu mengine yamebaki katika muundo wa kisheria na utekelezaji wa sheria zinazohusiana na ajira kwa mtoto, ikiwa ni pamoja na kinga kwa ushiriki wa mtoto katika shughuli haramu na kazi za majumbani; ukosefu wa idhini kwa wakaguzi wa kazi kufanya tathmini ya adhabu; na pengine kuwepo idadi ndogo ya wakaguzi wa kazi ikilinganishwa na ukubwa wa nguvu kazi ya Tanzania.

Kulingana na ripoti hiyo, hatua zilizopendekezwa zimetambuliwa na zingeendeleza kukomesha ajira kwa mtoto nchini Tanzania.

Eneo	Chombo Husika	Hatua Iliyopendekezwa	Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa
Muundo wa Kisheria	Tanzania Bara na Zanzibar	Haramisha uandikishaji wa watoto chini ya umri wa miaka 18 unaofanywa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali.	2016 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Hakikisha kwamba ulinzi kwa umri wa chini unatumika kwa watoto wote, wakiwemo wale wanaoshiriki kazi za majumbani.	2013 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Anzisha kisheria umri wa lazima kwa elimu, ambao hauachi mwanya kati ya umri wa lazima kwa elimu na umri wa chini kabisa kwa kazi.	2017 – 2019
	Tanzania Bara	Anzisha kisheria elimu bure ya msingi kwa umma.	2016 – 2019
	Tanzania Bara	Endelea kupanua orodha ya kazi zenye hatari sana na shughuli zilizopigwa marufuku kwa watoto ili kuhakikisha kwamba orodha hiyo	2016 – 2019

Eneo	Chombo Husika	Hatua Iliyopendekezwa	Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa
		inajumuisha kupalilia na kusindika katika uzalishaji wa tumbaku, karafuu, kahawa, katani na chai.	
	Tanzania Bara	Haramisha matumizi ya watoto katika shughuli haramu, hasa katika kutengeneza na usafirishaji dawa za kulevya.	2012 – 2019
	Tanzania Bara	Hakikisha kwamba sheria haipigi marufuku upatikanaji wa elimu kwa wasichana wajawazito na wavulana ambao hushiriki ngono.	2017 – 2019
Utekelezaji	Tanzania Bara na Zanzibar	Idhinisha wakaguzi wa kazi wa Tanzania Bara na Zanzibar kukadiria adhabu.	2017 – 2019
	Zanzibar	Rasimisha mafunzo ya wakaguzi wa kazi, ikiwemo kuwapatia mafunzo wakaguzi wapya wa kazi mwanzoni mwa ajira zao, mafunzo juu ya sheria zinazohusiana na aina mbaya sana za ajira kwa mtoto, na kozi za kunoa ubongo.	2019
	Tanzania Bara	Chapisha habari juu ya juhudi za utekelezaji wa sheria za ajira kwa mtoto.	2011 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Hakikisha kwamba afisa wa kazi aliyejitolea kwa dhati ameteuliwa kwa kila mkoa, na chapisha habari hiyo .	2013 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Ongeza idadi ya wakaguzi wa kazi ili kukidhi ushauri wa kiufundi wa ILO.	2013 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Toa ufadhili wa kutosha ili kuhakikisha utekelezaji wa kutosha wa sheria za kazi.	2013 – 2019
	Zanzibar	Rasimisha mafunzo ya wachunguzi wa utekelezaji wa sheria za jinai, ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa wachunguzi wapya, mafunzo juu ya sheria mpya zinazohusiana na aina mbaya sana za ajira kwa mtoto, na kozi za kunoa ubongo.	2019
	Zanzibar	Chapisha habari juu ya adhabu iliyotolewa kwa uhalifu unaohusiana na aina mbaya sana za ajira kwa mtoto.	2019
	Tanzania Bara	Chapisha habari juu ya mafunzo ya maafisa wa utekelezaji wa sheria za makosa ya jinai, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya wachunguzi wapya, mafunzo kuhusu sheria zinazohusiana na aina	2012 – 2019

Eneo	Chombo Husika	Hatua Iliyopendekezwa	Mwaka(Mi) Iliyopendekezwa
		mbaya sana za ajira kwa mtoto, na kozi za kunoa ubongo.	
Uratibu	Tanzania Bara na Zanzibar	Hakikisha kwamba kamati za uratibu zinafanya kazi na zina uwezo wa kutekeleza maagizo yao yaliyokusudiwa.	2018 – 2019
Sera za Serikali	Tanzania Bara na Zanzibar	Hakikisha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa juu ya Kutokomeza Ajira kwa Mtoto na Mpango wa Taifa wa Hatua za Kukomesha Manyanyaso dhidi ya Wanawake na Watoto nchini Tanzania.	2018 – 2019
	Tanzania Bara	Ondoa vipengele katika Mtihani wa Kumaliza Shule ya Msingi ambavyo ni vizuizi kwa elimu, kama vile sera ya kutofanya mtihani tena.	2016 – 2019
	Zanzibar	Jumuisha mikakati ya kuzuia na kutokomeza ajira kwa Mtoto, na hakikisha utekelezaji kamili wa Sera ya Elimu Zanzibar ili kupunguza wanafunzi kuacha masomo.	2018 – 2019
Mipango ya Kijamii	Tanzania Bara na Zanizbar	Hakikisha utekelezaji wa mipango ya kijamii inayofadhiliwa na serikali.	2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Imarisha juhudi za kuondoa vizuizi na pia fanya elimu ipatikane kwa watoto wote kwa kutokomeza au kulipa gharama kubwa sana zinazohusika, kama vile vitabu, chakula shuleni, na sare, huku ikihakikisha shule zina rasilimali za kutosha kwa wanafunzi wenye ulemavu na matatizo ya kujifunza.	2010 – 2019
	Tanzania Bara na Zanzibar	Unganisha mipango inayojumuisha ujenzi, uchimbaji madini, upasuaji wa mawe, kazi za majumbani, uvuvi, na sekta zisizo rasmi ili kushughulikia watoto wanaoshiriki ajira kwa mtoto.	2017 – 2019